

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**KIKAO CHA AROBAINI**

**01 JULAI, 2015**



# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA AROBAINI – TAREHE 01 JULAI, 2015

### I. MASWALI:

#### OFISI YA WAZIRI MKUU:

##### **288. MHESHIMIWA MODESTUS DICKSON KILIFI (MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Madiwani ni wasimamizi wa shughuli za maendeleo katika Halmashauri zetu nchini:-

Je, ni lini maslahi yao yataboreshwa ili yalingane na kazi wanayoifanya.

#### WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

##### **289. MHESHIMIWA MURTAZA ALLY MANGUNGU (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:-

(a) Je, ni kiasi gani cha mapato kimepatikana kutokana na gesi ya Kisiwa cha Songosongo tokea mwaka 1996 hadi sasa;

(b) Je, kwa nini Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa haipewi gawio (mrahaba) kutokana na uchimbaji wa gesi hiyo.

#### **290. MHESHIMIWA MOSES JOSEPH MACHALI (KASULU MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Katika Wilaya ya Kasulu hivi sasa kuna tatizo la uhaba wa nguzo za umeme pamoja na vifaa kama mita na nyaya za kuunganishia umeme kwa Wananchi kiasi kwamba kati ya megawati 2.5 za umeme unaozalishwa tangu mwaka 2011 ni takribani megawati 0.5 tu za umeme unaotumika:-

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kupeleka nyaya, mita na vifaa vingine ili kuhakikisha umeme kiasi cha takribani megawati 2 hakipotei kama ilivyo hivi sasa;
- (b) Je, ahadi ya Serikali ya mwaka 2013 katika mukutano wa Bajeti ya kupeleka umeme katika vijiji vya Nyumbigwa, Murufuti, Kidyama, Herujuu, Mganza, Ruhita, Kanazi n.k. imefikia wapi.

## **WIZARA YA UJENZI:**

### **291. MHESHIMIWA MOSHI SELEMANI KAKOSO (MPANDA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:- Barabara ya Kibo hadi Mwese inaunganisha Mkoa wa Katavi na Kigoma upande wa Magharibi; lakini jitihada za Mkoa wa Katavi ya kutengeneza barabara hii zimekuwa zikikwamishwa na Mkoa wa Kigoma:-

Je, Serikali iko tayari kuhakikisha eneo dogo la Mkoa wa Kigoma wanatenga fedha kwa ajili ya kufungua Mkoa huo.

### **292. MHESHIMIWA AL-SHAYMAA JOHN KWEGYIR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, kwa nini Serikali haibadilishi mizani ya magari nchini kwa kuondoa mizani za kukanyaga kwa “Exel” moja moja na kuondosha msongamano wa magari kwenye mizani hizo ambayo zina uwezo mdogo.

## **WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

### **293. MHESHIMIWA SALUM KHALFAN BARWANY (LINDI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Serikali imefuta hatimiliki za mashamba katika maeneo mbalimbali kwa wamiliki kushindwa kuyaendeleza kama ilivyotokea kule Tanga:-

Je, ni hatua gani zimechukuliwa hadi sasa kwa mashamba pori ya Lindi.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

### **294. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Hivi karibuni imesikika kwamba Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ndio lenye wajibu wa kupewa taarifa za ajali na maafa yote:-

Je, Serikali haioni kwamba Wananchi walio wengi hawajui ukweli huu na wanapopata maafa hukimbilia Polisi.

## **WIZARA YA FEDHA:**

### **295. MHESHIMIWA AMINA ABDULLA AMOUR (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:- Tanzania inategemea sana wahisani katika bajeti yake ya maendeleo na kila mwaka tunashuhudia wafadhili wakikataa kutekeleza ahadi zao kwa visingizio mbalimbali:-

Je, Serikali imejipanga vipi kuondokana na bajeti tegemezi.

### **296. MHESHIMIWA DKT. ANTONY GERVASE MBASSA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:- Kuna idadi kubwa ya wajane ambao wameondokewa na wenza wao ambao walikuwa watumishi katika Idara mbalimbali za Serikali ambao hadi leo hii hawajalipwa mirathi yao baada ya kukidhi taratibu na vigezo husika:-

- (a) Je, kwa nini wajane hao hawalipwi mirathi yao;
- (b) Vielelezo vinapowasilishwa huambiwa suala hilo linashughulikiwa; Je, shughuli hiyo huchukua muda gani hadi kukamilika;

- (c) Je, Serikali ina mpango wa kuanzisha kitengo cha mirathi katika ngazi ya Halmashauri ili kuwapunguzia gharama ya usafiri kufuata huduma hii Dar es Salaam.

## **II. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Kuwalinda watoa Taarifa za Uhalifu na Mashahidi wa Mwaka 2015 (*The Whistleblower and Witness Protection Bill, 2015*)

**DODOMA  
01 JULAI, 2015**

**DKT. T. D. KASHILILAH  
KATIBU WA BUNGE**